wote wakiwa wanafunzi wa shule ya msingi Matala.

Kwa mujibu wa Kamanda Maigwa,

Jongo.

Mbali na sababu hiyo, Kamanda huyo alitaja sababu nyingine kuwa ni baadhi kuogelea kwenye mito ambayo

Jaro, Simon Maigwa

miti Kituo cha Afya Mwanya Tarafa ya Olboloti akisema ni hatari kuvuka mito iliyojaa maji.

"Ninavyo vyombo vyangu vya usala-

*Imeandikwa na Daniel Mjema na Janet Joseph (Moshi), Susan Uhinga (Tanga) na Mohamed Hamad Kiteto*

MWANANCHI UK 17.

# Kuhamisha wauza samaki Moshi ngoma nzito

Daniel Mjema, Mwananchi
dmjema@mwananchi.co.tz

**Moshi.** Wafanyabiashara wa samaki na matunda katika soko la Manyema mjini Moshi, wametofautiana kuhusu uamuzi wa Serikali kuwahamishia soko la Pasua huku baadhi wakiafiki na wengine wakipinga.

Meya wa Manispaa ya Moshi, Juma Raibu alilazimika kujitokeza hadharani na kueleza upangaji wa wafanyabiashara si matakwa yake, bali ni utelekezaji wa maagizo ya Rais na yeye ni miongoni mwa watekelezaji.

Suala la kuwahamisha wafanyabiashara hao kwenda soko la Pasua mjini Moshi linapingwa na baadhi ya wafanyabiashara wakidai soko hilo si rafiki kwa biashara.

Tayari Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Stephen Kigaigai aliingilia kati sakata hilo na kuweka msimamo wa Serikali kuwa ni lazima wafanyabiashara hao waende katika soko la Pasua.

Baadhi ya wafanyabiashara wa samaki walisikika wakidai kuwa kama Serikali itawalazimisha, hawatakwenda na watauza samaki kwa siri eneo la Fonga Geti au kuwaelekeza wateja wao kwa simu walipo au wao wawafuate walipo.



Wafanyabiashara wa samaki wakiendelea kuwahudumia wateja katika soko la Manyema, licha ya kutakiwa kuondoka na kuhamia soko la Pasua kupisha ujenzi wa soko la kisasa. **Picha na Dionis Nyato**

### Meya Moshi afunguka

Pamoja na msimamo huo, baadhi ya wafanyabiashara katika soko la Manyema walimshikia bango Meya Raibu, hali iliyomfanya ajitokeza na kusema anasakamwa kwa sababu ya utendaji kazi wake haupendezi baadhi ya wenzake.

"Februari 22, 2022 nimeona baadhi ya wafanyabiashara wa samaki katika soko la Manyema waliandamana hadi ofisi ya CCM Moshi mjini wakipinga uamuzi wa Serikali wa kuwahamishia soko la Pasua ambalo lina miundombinu yote.

"Ninafahamu kuna baadhi ya wafanyabiashara na viongozi wa CCM wako nyuma ya hili kwa sababu wana maslahi yao pale Manyema. Uamuzi huu si wa meya, bali ni wa baraza la madiwani Manispaa ya Moshi," alisema na kungeza:

"Namshukuru RC kwa kuingilia kati hili na kulieleza vizuri kwa vile yalikuwa ni maamuzi ya vikao halali na makabrasha yapo. Baada ya kauli ya RC tayari wafanyabiashara wa samaki wameenda Pasua na kuanza kujiandikisha."

Nasibu Mariki, Diwani wa Kaloleni ambaye pia ni mwenyekiti wa Kamati ya Mipango Miji na Ardhi, alisema suala la kuwahamishia wafanyabiashara hao ni uamuzi wa baraza la madiwani na si uamuzi wa mtu mmoja. Mwenyekiti wa Kamati ya Huduma za Jamii ya Halmashauri hiyo ambaye pia ni Diwani wa Mji mpya, Abuu Shayo alisema kamati ya usalama ya wilaya ilishatembelea soko hilo na kujiridhisha ni bora na safi.

> **"Mwanzo nilikuwa na wasiwasi, lakini baada ya kulitembelea nimeona liko vizuri. Kama wafanyabiashara wote tukihamia biashara itachanganya kwa sababu wateja watatufuata."**
> Christina Daud

### Wafanyabiashara watofautiana

Christina Daud, alisema baada ya kutembelea soko la Pasua na kujionea miundombinu, wasiwasi aliokuwa nao umeondoka, hivyo kuwaomba wenzake wasipinge kabla ya kuona.

Kauli hiyo iliungwa mkono na Rajabu Balozi aliyesema amejiridhisha na miundombinu na mazingira ya soko hilo na alishajiandikisha kuomba kupatiwa kizimba cha kuuzia samaki.


Hata hivyo, Joseph Martin alidai biashara katika soko la Pasua ni ngumu na itakuwa usumbufu na gharama kwa wateja kupanda daladala zaidi ya mbili na kwamba hata meya alifungua biashara ya M-pesa ikamshinda.

Mfanyabiashara mwingine, Twaha Sadiki alihoji kwanini wafanyabiashara wa samaki ndio wanaosumbuliwa na kueleza huo ni uhamisho wa saba tangu aanze biashara hiyo.

Scanned with CamScanner

*MWANANCHI UK 24*

# a neno Kibaha



ya Rais (Tamisemi), Innocent Bashungwa akizungum- Shule ya sekondari ya wavulana ya Kibaha ambayo iko mu Kibaha, wakati wa ziara yake iliyofanyika mkoani

yi kama shirika ngea mazingira kuwafundisha taasisi nyingine usaidia" alisema a.

ingine ambazo uzifanyia kazi- na kuwawekea shi wahitimu kulingana na

taaluma zao kwa kujenga maeneo ambayo watakuwa na uwezo wa kuyafanyia kazi, huku halmashauri zikiwawezesha katika mikopo ya asilimia 10.

"Hao watu wa nchi za Nordic waliotusaidia kipindi shirika hili linaanzishwa naweza kuwaita waje watusaidie ili tufike mbali zaidi kikubwa anzeni," alisema.

# aka mchakato ni kwa wazee

03

nbao Sera ya Wazee a na Serikali.

masikini pamoja zee, lakini kama o katika hatua za isha inakua na wa pensheni kwa

a la pensheni kwa ni muhimu sana atika nchi nyingi kwa katika she- linatekelezwa na pa Tanzania kwa wa Zanziba tayari aji umeanza na a miaka zaidi ya ambapo wazee miaka 70 hulip- sheni kila mwezi, ata huku Bara hilo linahitajika la ya wazee wetu i" alisema nua kuwa tayari

Bunge baada ya kupitishwa kwa sera ya wazee ya mwaka 2003, lilishajadili suala la pensheni kwa wazee na kuipitisha na kilichobaki na wizara kushirikiana na Bunge kupata miongozo itakayowasaidia kutengeneza kanuni kuwezesha wazee hapa nchini kuanza kunufaika na mpango huo wa pensheni.

Mkurugenzi mkuu wa shirika hilo hapa nchini Smart Danieli licha ya kuishukuru Serikali kwa hatua kubwa iliyofikia katika jitihada za kuhakikisha inawasaidia wazee hapa nchini , alisisitiza kuhusiana na suala la kipato kwa wazee.

Danieli alisema kutokana na changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wazee hapa nchini ni wazi suala la pensheni linahitajika kwa haraka.

# Kiwanda cha ngozi chaanza

Mwandishi Wetu, Mwananchi

Kilimanjaro. Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu anayeshughulikia Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu Profesa Joyce Ndalichako amepongeza uwekezaji kati ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) pamoja na Jeshi la Magereza Tanzania kwa hatua nzuri ya ukamilishaji wa kiwanda cha uzalishaji bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro.

Waziri Ndalichako alitoa pongezi hizo Februari majuzi baada ya kupokea taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa kiwanda hicho wakati alipokitembelea kwa lengo la kukagua maendeleo na kuangalia namna ya uzalishaji wa bidhaa unavyofanyika

"Kiwanda kimefikia hatua nzuri na mashine zote zimeshafika, hatua inayoendelea ni kuziunganisha mashine hizo ili uzalishaji uendelee kufanyika. Viatu vinavyotengenezwa hapa ni vizuri na wanatengeneza viatu vyenye mitindo ya aina mbalimbali," alisema Profesa Ndalichako.

Aliongeza kuwa, uwepo wa kiwanda cha bidhaa za ngozi cha Kilimanjaro, utachangia kwa kiasi kikubwa kupunguza tatizo la ajira nchini mara tu baada ya kukamilika kwa kiwanda hicho.

"Kiwanda kina uwezo wa kuajiri watu zaidi ya 10,000 ambapo ajira za moja kwa moja ni 3,000 pamoja na ajira zaidi kwa Watanzania kutokana na fursa mbalimbali zitakazo kuwepo kiwanda hapo," alisema

Aidha, Waziri Ndalichako aliwasihi watendaji wa kiwanda hicho kuhakikisha malengo ya uzalishaji katika kiwanda, yanazingatiwa ili fedha zilizowekezwa zitumike kwa matokeo yaliyokusudiwa.

Sambamba na hayo alipongeza uongozi wa Chuo cha VETA pamoja na Taasisi ya Teknolojia Dar es salaam (DIT) kwa kutoa mafunzo bora kwa vijana ya utengenezaji wa bidhaa za ngozi, huku akibainisha kuwa vijana wanaotoka katika vyuo hivyo wamekuwa watengenezaji wazuri wa viatu.

Naye Mkurugenzi mtendaji wa Kiwanda cha bidhaa za Ngozi cha Kilimanjaro, Mhandisi Masud Omary alieleza kuwa menejimenti ya kiwanda hicho imejipanga kuendelea kukuza masoko ya bidhaa zinazozalishwa kiwandani hapo, ili kuhamasisha wananchi kununua bidhaa hizo. Pia alieleza juhudi zinazofanywa na kiwanda katika kukuza soko la bidhaa nje ya nchi.

Scanned with CamScanner

* NIPASHE UK 9 *



# Madiwani sasa wataka elimu alama za mifugo

**Na Shaban Njia**, KAHAMA

MADIWANI wa Halmashauri ya Ushetu wilayani Kahama mkoani Shinyanga wameishauri serikali kupitia idara ya mifugo kutoa elimu kwa wafugaji juu ya umuhimu wa alama katika mifugo yao.

Wameitaka elimu hiyo kabla ya kuanza zoezi la kuweka mifugo alama za hereni ili kuleta ufanisi na tija katika utekelezaji wa agizo hilo.

Hayo yalibainisha na madiwani wa halmashauri hiyo katika kikao cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/23 kilichokuwa kinajadili taarifa mbalimbali za maendeleo, ikiwamo hali ya ukusanyaji wa mapato ya halmashauri hiyo.

Diwani wa Chambo, Daudi Mahona, alisema, wafugaji hawajaelimishwa kuhusiana na zoezi la kuweka alama katika mifugo yao hivyo ni budi serikali ikaweka utaratibu wa kukutana nao ili kuwaeleza kinaga ubaga kuhusiana na faida za kuweka alama za utambuzi kwenye mifugo yao hali itakayosaidia kuondokana na wizi.

"Sisi madiwani hatujapewa elimu juu ya umuhimu wa kuweka alama za utambuzi (hereni) ng'ombe, mbuzi na kondoo kama serikali inavyotaka, bei zake ziko juu ikilinganishwa na zoezi la awali ambapo walikuwa wanalipia Sh. 500 kwa ajili ya kuwekewa chapa," alisema Mahona.

Naye Diwani wa Bukomela, Kulwa Shoto, aliiomba serikali kuwapunguzia wafugaji bei za kuweka hereni kwenye mifugo ambapo kwa sasa ng'ombe mmoja mfugaji analazimika kulipia Sh. 1,750 huku mbuzi na kondoo ikiwa ni Sh. 1,000, bei ambayo iko juu zaidi.

Alisema mwaka jana walikuwa wakiweka chapa kwenye mifugo kwa Sh. 500 kwa kila mfugo mmoja na ilileta shida kwa wafugaji na kushindwa kujitokeza zaidi na baadhi ya mifugo ilikufa kwa kuweka vibaya alama na sasa wanakuja na bei mpya kabla ya kuanza kutoa elimu juu ya umuhimu wa zoezi hilo.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema, busara inapaswa kuzingatiwa kabla ya kuanza utekelezaji wa zoezi hilo la kitaifa.

Awali akitoa ufafanuzi wa suala hilo, Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Mwalimu Linno Mwageni, alisema, serikali kupitia imetoa maelekezo juu ya uwekaji wa alama mpya za utambuzi wa mifugo ili kudhibiti vitendo vya wizi wa mifugo na upotevu wa mifugo mara kwa mara.

# Mak
# yak

**Na Yasmine Prot**

HALMASH
Kinondo
kopesha
kundi 2,8
na watu wenye
2017 hadi 2022.

Hayo yalisemw
Jamii wa Manisp
ipokuwa akitoa
Maendeleo na Ji
na Mtandao wa Ji

Alisema, manis
jitihada mbalim
uwezo na kuwa
wake kwa kuwa
asilimia 10 ya ma

"Katika kufani
2017 hadi 2022
12,186,429,539 z
vikundi 2,845 vy
wenye ulemavu.

Alifafanua ku
ispaa ilikopesha



# Uha

**Na Neema S**

SHULE ya
Bulungwa, H
Kahama, ina
ya vyoo, ha
hasa kipindi

Shule hiy
1,383 ina n
vyoko ni 11
inayowapa
mapumzikc

Hayo yal
wa shule
harambee
viwili vya
unafadhili
hiyo.

Alisema
masika w
mashamba

Kwa muj

Scanned with CamScanner

kwenye matokeo ya kitaifa ya mtihani wa kidato cha pili mwaka jana. (Picha na Mpiga Picha Wetu).



Alisema taasisi hiyo imekuwa ikitoa mafunzo hayo kwa kipindi cha miaka10 yakilenga kwa wakurugenzi wa bodi wa taasisi na mashirika ya serikali na binafsi kuweza kujiendesha kwa misingi ya utawala bora.

RAIA MWEMA UK 16

# Ng'ombe kuvalishwa herein za kieletroniki

**Na Joseph Ngilisho Arusha**

**HALMASHAURI** ya wilaya ya Arusha (Arusha DC), imeanza zoezi la utambuzi wa mifugo kwa kuzivalisha Ng'ombe hereni maalumu za kielektronoki na kuzisajili kwenye mfumo wa kitaifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri ya Arusha DC, Msumi Selemani, ameyasema hayo alipokuwa akielezea utekelezaji wa mpango huo wa kitaifa wa zoezi la kusajili mifugo kwa kutumia mtandao kutokana na zoezi kuwa na manufaa kubwa.

Alisema ili ng'ombe hizo zitambulikane na kufahamika idadi yao na kuachana na matumizi ya chapa ambayo huharibu ngozi,wameamua kuja na mfumo huo wa kieletroniki.

Selemani amewashauri wafugaji wote kuhakikisha wanashiriki kikamilifu kwenye zoezi hilo la kusajili ng'ombe kwa kuwavalisha hereni na kuacha kabisa matumizi ya chapa ambayo inaharibu ngozi ya mifugo na kuikosesha thamani

Akielezea utekelezaji wa mpango huo Mganga wa Mifugo wa Halmashauri ya Arusha DC, Dk.Linus Prospal, alisema zoezi hilo ambalo lilizinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, limeanza kutekelezwa mwezi Desemba mwaka jana na litafikia mwisho mwezi Augosti mwaka huu

Alisema kuwa usajili wa ng'ombe kwa kutumia teknolojia hiyo ya kisasa ya kuvalisha hereni, itawezasha kusitisha kabisa matumizi ya chapa ambayo huwa inaharibu ngozi na kuikosesha thamani, kufahamu idadi ya mifugo hiyo na maeneo ilipo na ikitokea wizi itapatikana kwa urahisi kwa kuwa itaonekana kwenye mtandao.

Dk. Linus aliyataja manufaa mengine kuwa ni mfugaji kulipia bima ya mifugo, atapata ruzuku, mikopo na kuondoa migogoro kati ya wakulima na wafugaji kugombea maeneo ya malisho na kilimo na maji

Alisema wamekuwa wakitoa elimu kwa wafugaji kuacha kabisa matumizi ya chapa na badala yake wasajilj mifugo yao kwa kutumia teknolojia hiyo, kufuga kisasa sanjari na kutunza mazingira kulima malisho ya mifugo ili wakati wa kiangazi wasitaabike kusaka malisho.

Msimamizi wa zoezi hilo la utambuzi, ukaguzii wa nyama, usajili na ufuatiliaji Halmashaurii ya Arusha DC, Dk. Yohana Kione, alisema kwenye zoezi hilo la usajili wa mifugo lina faida nyingi zikiwemo kupata masoko ya ndani na nje.

Scanned with CamScanner